Galgalo Gurguro: Shukrani kwa mkutano huu. Mkutano huu wa Kenya, this is Kenya, mimi niko miaka 76. Tangu wakati wa ukoloni mimi mzaliwa wa Kenya. Mzaliwa wa Kenya lazima katika Katiba ambayo inakuja yote sisi tuko hapa. Katiba hii na shukurani kwa ajili ya Katiba hii mimi nasimama. Kwa hivi mabadiliko mingi imekuja tangu Kenya ilipata uhuru. Wakati Kenya ilinapata uhuru, mimi nilikuwa askari, sina masomo mengine, masomo yangu ni ya kuchunga ng'ombe na mbuzi lakini wakati niliingia nikapata kazi ya askari, nilipata masomo kidogo.

Tafadhali Serikali yetu ya Kenya ikubali kitu kimoja, ile sheria ya zamani, ni sheria nzuri. Vile mtu mmoja amesema mbele yangu, mimi naunga mkono. Tena ni nafasi yangu ya kusema sasa kitu moja; mwenye kuchunga ng'ombe anajua hali ya ng'ombe, mwenye kuchunga shamba anajua hali ya shamba, mwenye kuchunga miti anajua hali ya miti na mvua. Sisi tunajua hali yetu ya ufugaji. Sasa katika watu waliokuwa jirani wetu, jirani wetu ni Meru, Samburu, Somali, Ogaden jirani wetu ni watu tatu

Com. Lethome: Tukaeni kimya tafadhalini tumsikize mzee, tafadhalini.

Galgalo Gurguro: Jirani wetu walikuwa watu watatu. Watu wetu walikuwa zamani hapa wauawa, Samburu wanachukua ng'ombe moja, mimi nikipata ninashika ile ng'ombe narudisha. Hakuna matata wale wanauana. Sasa, siku hizi vile unaona wakati hata mtu anauawa na hakuna hatua kwa sababu ile imechukuliwa na hakuna kufuata (inaudible) halafu unafanya ile mtu ana question mtu mwingine akuje (inaudible). Hii ni sheria ambayo sisis hatuwezi. Sababu hiyo sheria haiwezi kuleta usalama wa mtu, haiwezi kuleta usaidizi wa mtu ile ya kuunganisha watu, hii ni mbaya.

Ya pili, sisi tena katika province hii, Kenya kuna province nane, sasa sisi ni watu wa kufuga, watu wengine ni wa shamba na tunaunganishwa pamoja. Mimi nataka kama Serikali yetu inatusikiza, province yetu iunganishwe watu wa ng'ombe, watu wa ngamia, watu wa mifugoya mali hawa ndio wanaweza kusikizana. Kwa sababu hii ng'ombe yetu inatoka hapa inakwenda Nairobi, hii si hile biasharafaster mimi nasukuma. Nasukuma na gari, ile biashara nimepate, ile faida ya ng'ombe, hakuna ng'ombe iko faida, mbuzi hakuna faida, ngamia faida, sisi hatuna barabara. Ng'ombe inaweza lala dakika ngapi hapa katikati hii? Imechoka kutembea (inaudible) ile (inaudible) mpaka Nairobi, uchungulie. (inaudible) sio karibu ya nini, upate karibu na mahali pa kufuga. Hii ni faida yetu mzuri. Tena watu wanauawa na hakuna damu, kama huna kitu. Leo unauwa, kesho unauwa kwa sababu hawashikwi, polisi washike wale watu na wafungwe. Sasa wanawachiliwa wanachukua mali, ng'ombe na hakuna kitu ambacho kina faida. Sisi tunataka Kenya, hii province yote vile watu wanaendelea, inafaa wakae pamoja. Salaam Aleikum

Com. Lethome: Swali moja mzee, ngoja kidogo, umesema ng'ombe ikichukuliwa, mtu akiuliwa, polisi achukuwe hatua na akikataa kuchukua hatua unataka polisi tumchukulie hatua gani?

Galgalo Gurguro : Hatua hio.

Com. Lethome: Mwambieni kwa Kiborana.

Speaker: (inaudible)

Galgalo Gurguro: Hii itakuwa malalamiko.

Com. Lethome: Kwa nani?

Galgalo Gurguro: Lalamiko kwa Serikali.

Com. Lethome: Polisi ni Serikali?

Galgalo Gurguro : Ndio.

Com. Lethome: Sasa ulalamike kwa Serikali tena?

Galgalo Gurguro : Hapana, lalamiko kwa mwanasiasa.

Com. Lethome: Kwa mwanasiasa?

Galgalo Gurguro : Eh, wale watu wamechagua

Com. Lethome: Haya asante. Nataka mfikirie hilo, wale wengine ambao hamjatoa maoni, fikirieni hio. Ikiwa mtu katika Serikali, ofisa wa Serikali hatimizi kazi yake, achukuliwe hatua gani? Be thinking about that halafu mtatoa maoni yenu. Aah, fikiria halafu utasema baadaye. Mohammed Diba

Mohammed Diba: Salaam Aleikum. Mimi ni Mohammed Diba Wario, I am here to represent the Constitutional review proposals on Judiciary, local Government and electoral system and processing. I will start with the Judiciary. The present structure of Judiciary is adequate for Kenyans; however, the judicial officers are to be appointed by the judicial service Commission with university graduation as their qualification. Judiciary consists of subordinate courts, the magistrate court, the

high court, the Kadhis court and the court of appeal. In conjunction with this, the new Constitution should establish human rights court.

Regard to this court, the chief kadhi is to be appointed by the Muslims with completion of Faculty of Sheria in an Islamic university. All holders of Constitutional offices; attorney general, judges, public service Commission, electoral Commission, controller, auditor should enjoy security of tenure within their offices.

Local Government, since they are the closest to the people, local authorities are the most basic level of Government. Therefore, mayor and council chairman to be directly elected by the people. Elected candidates to be elite 'O' level and above. The remuneration of the councillors should be determined by the Parliament. Council should be independent to run their affairs from central Government. The local government chapter 265 be reviewed to empower the councillors in managing the affairs of the council and municipality. 75% of taxes, natural resources and wealth generated within the district be managed by the local councillors for the development of their own districts.

The electoral system and processing. The current representative electoral system is to be retained in Kenya, the desired system. One, to retain simple majority rule as a basis of winning an election. No nomination of any person who was rejected in the election. Vice should be elected by the Parliament. All appointees should be passed by the Parliament. Parliament is the lawmaker; during the process of law making 75% of the Parliament should be present to pass the law. Civic, Parliamentary and local elections should be done at different intervals or should be done at different times, President, MPs and councillors respectively. Counting of the votes should be done at the respective wards; there is no way that they will be taken to the districts. The new Constitution should impose heavy financial penalties on MPs wishing to defect between general elections. DC should not be a nominated councillor. Finally, nomination of MPs and the councillors to be abolished.

Com. Lethome: Can you repeat again the VC should not be a nominated what?

Mohammed Diba: DC should not be a nominated councillor because in our district

Com. Lethome: Councillor?

Mohammed Diba: Should not be a nominated councillor. In our district

Com. Lethome: District Commissioners?

Mohammed Diba: District Commissioners.

Com. Lethome: Should

Mohammed Diba: Should not be a nominated councillor

Com. Lethome: Just a minute, is the DC a councillor?

Mohammed Diba: Yes, he is being taken as a nominated councillor in the district.

Com. Lethome: Okay.

Mohammed Diba: He is the head of the district and thus he is being appointed as a nominated councillor

Com. Lethome: So he should just remain as a?

Mohammed Diba: As a DC.

Com.Lethome: Okay fine, thank you. Thank you very much kwa hayo maoni mazuri sana, sasa tuna fanya affirmative action kidogo, Halima Golo, women forum.

Halima Golo: Salaam Aleikum?

Audience: Aleikum Salaam.

Halima Golo: Salaam Aleikum?

Audience : Aleikum Salaam.

Halima Golo: Mimi naitwa Halima Golo, I am representing Women Forum, Merti Division. The new Constitution should provide the following for women, especially pastoral women; one, participation of pastoral women in decision-making forum. Two, pastoral women should have equal rights and opportunities in access to education and economics. Pastoral women should have equal sharing powers and leadership, e.g. chief and head of institutions.

Both parties intending to marry should be given equal opportunities in decision making. Early marriage should be condemned; appropriate age of marriage should be above 18 years. Pastoral women should have equal rights to inherit and have control of property e.g. livestock especially in our area. Traditional women inheritance practise should be condemned.

Incase the spouse dies; women should not be inherited by anybody as this will encourage HIV/AIDS. A woman should be recognized as human but not as property. Women and men intending to marry should go for HIV test. Female genital mutilation practise should be discouraged and stopped because this may cause even death. Both men and women should be given opportunities to decide when to have children.

Pastoral woman should not be tied to the traditional practises and religion to decide her destiny. Pastoral women should be given basic necessary information that matters to their maternal life e.g. encouraging them to deliver at health institutions. To encourage pastoral girl child education, the state should establish specific scholarship for pastoral girl child. Girl child labour should be discouraged. The state, in this case should ensure that any interference with the girl child rights should be punished. The state should recognise women as potential responsible and assets to the state/community. Lastly, the state should strengthen the law that governs the family welfare.

Com. Lethome: Asante, swali moja tu, umesema kuhusu ndoa ya mapema ipigwe marufuku. Sasa tungependa, unajua sheria, you have to give the law some teeth, sheria lazima uipatie meno ya kuuma. Sasa mtu ambaya atamlazimisha mtoto wa kike kutoka skuli halafu amuoze, ungependa sheria imuume namna gani? Ipatie sheria meno kidogo.

Halima Golo: Sheria itatue halafu ichukue hatua ambayo inafaa.

Com. Lethome: Yaani kwa mfano baba akimlazimisha msichana wake aolewe, kama yeye msichana mwenyewe hataki, apelekwe kotini ashtakiwe ama?

Halima Golo: Yeye apelekwe kotini na hatua ifaayo ichukuliwe.

Com. Lethome: Na huyo bwana ambaye anataka kumwoa msichana?

Halima Golo: Hata bwana pia kwa sababu ana fanya makosa kuoia msichana kabla miaka yake ya kuolewa imefika.

Com. Lethome: Okay. Haya Asante. Tunapata affirmative action nyingine tena Halima Ali. Karibia Halima

Halima Ali: Salaam Aleikum?

People: Aleikum Salaam

Halima Ali: Mimi nafikiri yangu ni machache, siongei mengi lakini ningeongea mengi kwa sababu vile mimi, nikisema mimi si mimi peke yangu lakini vile wakina mama wako na shida, ningeongea mengi zaidi. Lakini kwa vile sijui muda inaweza

kuturuhusu, mimi nitaongea juu ya shida ya kina mama. Wakina mama vile wale ambao walikuwa wameongea mbele yangu wanasema, tunaolewa mapema. Sisi wakina mama ile shida tuko nayo, tunaolewa mapema, tukiolewa mapema tutoke kwa boma ya baba, wakati tunatoka kwa boma ya baba hatutoki na chochote. Tunatoka mwili tu hata mavazi tunawacha kwa nyumba tunatoka na ya mwanaume. Tukifika kwa boma ile ya mwaname, tukizaa naye mtoto, baada ya kuzaa, mapenzi yetu ikiisha tunaambia toka tukitoka, tunatoka na nguo ambaye tulikuwa tumetoka nayo kwetu ndio tunarudishwa nayo. Hatuna mali yoyote, hatuna boma, hatuna ploti, hatuna ng'ombe wala nini na nini. Kama ni kutafuta mali. Mpaka nguo ambayo tulikuwa tumetoka nayo kwetu ndio tunarudishwa nayo. Hatuna mahali yoyote hatuna boma, hatuna ploti, hatuna ng'ombe wala nini na nini. Kama ni kutafuta mali tayari tulikuwa tumetafuta pamoja mpaka mwisho tumeipata. Haya baada ya kupata hiyo mali tukifukuzwa tunakuja pengine tuzae mtoto tuwe na watoto, tukiwa na watoto tunanyanganywa mwanaume anasema ya kwamba mtoto ni wake, watoto ni wangu ati waninyanganye.

Mimi mama ile nimebeba miezi tisa kwa tumbo yule mtoto tayari nimenyanganywa na ule uchungu ambao nimeskia yule bwana hata hajasikia lakini tayari amepata mtoto amezaliwa, na amelelewa vizuri, na ndio huyu anatembea hana shida yeyote anaona mtoto huyo ni wake, na nikiuliza maswali ninyi wamaume vile muko, huyu mtoto angekuwa ni wa nani? Nani alikuwa na uchungu wa huyo mtoto?

Interjection Com. Lethome: Pendekezo, unapendekeza awe wa nani?.

Halima Ali: Kama ni mimi napendekeza mtoto angekuwa ni wa mama kwa vile yeye ndiye amebeba mwezi tisa, na vile amepata hiyo bwana hana habari ilipatikana. Kwa hivyo vile nimependekeza kama ni mimi ninaulizwa ama akina mama wengine wakiulizwa mtoto angekuwa ni wa mama. Na kama ni kulelewa mtoto bwana akiwa na nguvu kuliko ile mama azaidie kulea ile mtoto, nguvu yake ikipatikana asikule peke yake, akule na mama pamoja, sio anatupa mama nyuma ya fence na tayari anakula chakula ile mtoto amelea. Na ya pili sisi wakati tuna kuja vile nilisema tunakuja kivyetu, tukifukuzwa na tumechukuliwa tukiwa wadogo tumezeeka huko kwa hiyo boma, tukitoka hiyo mahali tutatoka na nini na tayari tumetoa mbegu ya kutosha iko chini yote na tumenyanganywa hiyo mbegu tutaenda na nini kuisaidia tena ukiwa tumenyanganywa nguvu yetu?

Interjection Com. Lethome: Pendekezo, pendekezo unataka utoke na nini huko?

Halima Ali: Kwa hivyo tunataka kile tumepanga na yeye tumeaaidiana atuwachie ama tugawanye atuwachie kiasi na yeye abaki na kiasi. Hiyo ndiyo tunataka. Na ya pili ya tatu sisi tukikaa hivi kwanza wacha upande ya down country hata ni tofauti kubwa sana sisi watu pengine hawana habari, tunasikia huko wanawake wanapelekwa nje mara ingine wanafanyiwa sijui nini na nini, sisi hapa tunasahaulika.

Wacha kitu ingine, maofisa wetu ambao ni wanawake ambao tuko hapa tukisema kitu kikipangwa namna hii wanaume wanatangulia wanakaa huko nyuma wanatufinya hata wacha wengine nje hapa wenyewe, tunakuwanga. Ma ofisa zetu hata

kama iko mkubwa kuliko sijui nani anakuwanga nyuma. Sijui kwanini hatupata kitu ambaye wanapata mbele, sisi tunapata nyuma hapa enyewe tuko na shida. Ya pili mwanamke akijitoka akitaka kusema maoni, hayo maoni yake yanakanyangiwa tunastushwa mpaka roho yetu tayari wanatunyanyasa ndani ya nyumba tunastuka hatuwezi kutoa hapa hivi.

Interjection. Com. Lethome: Hapana leo, leo tumesema tangu mwanzo hakuna mambo ya kushtuliwa na mtu, hakuna polisi ya kukushtua, ama mzee wa kukushtua. Mama toa maoni yako kwa uhuru na kama, nawaambia hivi kina mama, kama kuna maoni ambayo munataka kutapatia separately mahali tutapanga kikao kando mtuambie yote bila uwoga. Lakini hakuna mtu atakushtua hapa toa yote hapa.

Halima Alir: Sawa sisemi saa hizi, sisemi saa hizi mimi si mtu wa kushtuliwa siwesinikastuka. Ya pili, tena mwanamke bwana wakati hayuko either msichana kama ako, msichana tuseme kama kwetu sisi huwa tunachunga, tukichunga mwanaume anakuja yule ako na nguvu anarape mwanamke, akirape mwanamke sisi tunakaa chini ya mti tuu huyo mwanamke amerapiwa huyo mwanaume hajulikani ako na shida gani. Wanachukua ng'ombe hiyo maneno inaisha na pengine mtu tayari anaweza kuwa na ugonjwa fulani mwanamke ndio huyo amepata ile ugonjwa. Watu yake ama wale wazee wanaongea wamechukua ng'ombe sasa hiyo ng'ombe inafaidi huyo mwanamke ama inafaidi hiyo family?.

Com. Lethome: Sasa unataka mtu akirape achukuliwe hatua gani?

Halima Ali: Hiyo, hiyo mimi kwa upande wangu nafikiri hakuna tofauti na yule ameua. Kwa hivyo hata yeye auwawe.

Com. Lethome: Sawa.

Halima Ali: Ndio. Mimi yangu ni hayo. Kwaheri.

Com. Lethome: Asante mama, hebu ngojeni kina mama wale ambao munasimama huko nyuma tulikuwa tumetenga pande hii kina mama wakae hapa. Kwa hivyo kina mama huko kuna nafasi yenu hapa ya kukaa chini, msikae nyuma huko njooni mkae hapa mbele kina mama. Okii sijui Okii nani? Diba, Okicha Diba yuko? Haya karibu Okicho. Alafu kaeni kimya tafadhalini, tukaeni kimya tumsikise Okicha.

Okicha Diba: Asanteni sana. Mimi jina langu ni Okicha Adilo Ibrahim. Nafikiri mengi watu wamezungumza mbele yangu lakini chache nitasema. Yale nitasema machache, ya kwanza watu wanaongea juu ya mpaka, amri ile ya mpaka nafikiri wanaguzaguza wajaweka sheria yao vizuri kwa maoni yangu. Maoni yangu nafikiri ninaona kama ni mpaka area yetu Wazungu walichora map hawakuchora eti wanapendelea Borana ama kabila ingine yoyote. Walichora map hiyo kulingana na vile tulikuwa tunaishi, nafikiri tunataka kuwa tuwekewe mkazo hiyo ardhi iwe na dhamana mtu asiguze, mtu aziguze ni njia gani je? Nafikiri kwa upande yangu sio bunduki hii ya sold nini na nini, tupatiwe bunduki mzuri kama mfano ile ya kama (Inaudible) watu wanakuwa

na G3 wanagawiwa wanachunga mali yao. Nafikiri tunataka tupatie kwa mpaka yetu bunduki mzuri ambayo inaweza chungu ardhi yetu huko. Na mpitishie hiyo.

Com. Lethome: Sasa bunduki mpatie polisi ama raia?

Okicha Diba: Raia, achunge area heri, ili mtu asikanyange, hiyo maoni yangu namna gani tunaweza.

Com. lethome: Maoni yake, maoni yake hayo sawa hiyo ni maoni yake.

Okicha Diba: Ya pili. Nasema hii mambo ya mifugo iwe na dhamana, mifugo iwe na dhamana namna gani? Mifugo iwe na dhamana na kama njia, kama hatuna njia yoyote, kama njia yote, sawa sawa. Kama hatuna njia tunataka tuwekwe kama province ile unasema tuwe na province hata yetu kando ni hakuna maana kama hatuna, hakuna maana kwenda kando na watu wengine kama hatuwezi fanyiwa lolote wanasema wanapanga hawezi fanya. Kama watapanga tunakuwa na ardhi yetu na amri yetu yote inasikizwa.

Interjection. Com. Lethome: Ebu tukaeni kimya tafadhali huko nyuma mnazungumza sana.

Okicha Diba: Ya pili, afadhali tuwe na tuwekewe sawa na wengine, sawa na wengine tuwe na lami, kama kukiwa lami mpaka huko pale kwa mpaka. Kama tuko na lami tuko na ardhi. Sasa ardhi yetu haina dhamana, hakuna hatujulikani, hiyo amri iangaliwe kama tunachagua mbunge, mbunge sio ati ana, atakuja na nini, njia hakuna, hakuna mahali ataenda, hakuna njia. Afadhali amri hiyo iwekwe tuwe halali tunaweza kuwa sawa na wengine ndio tunaweza kuwa na process kando. Lakini watu iko mbali na watu taweza pata kitu gani tuwe kama wengine? Afadhali turekebishwe kwanza kila kitu ndio utaweza kujiangalia tulikuwa, tunaweza kuwa kando na wengine. Ya pili.

Com. Lethome: Hiyo siyo ya pili ya tatu sasa.

Okicha Diba: Ya tatu tangu shifta, tangu zamani nilikuwa nimezaliwa mbele ya vita ya shifta niliona, sisi hatuna umaskini lakini tumeingiliwa na umaskini tumekuwa maskini mbaya zaidi. Je, tuwekewe haki gani? Tumedhulimiwa haki gani inaweza kurudishiwa sisi? Tuwe kama Zamani.

Com. Lethome: Wewe pendekezo unataka nini ifanywe ndio muwe kama zamani.

Okicha Diba: Tuwe kama zamani? Ya kwanza ardhi yetu mtu asikanyange, ya pili Serikali irudishe mali yetu ile kwa kila moja ambaye walipata damage.

Com. Lethome: Sawa. Haya endelea. Tafadhalini mpeeni nafasi atoe maoni yake, endelea.

Okicha Duba: Hiyo ni ya tatu si ndio?

Com. Lethome: Ee hiyo ni tatu sasa nne.

Okicha Duba: Ya nne. Tunasema, mambo ya province, je, kama sisi tuko na MP ama Councillors na hatuoni wa kusimamia hapa, tunaweza kuwa sawa na wengine namna gani? Yeye awe na sisi kila wakati, kila wakati sio kama sasa (inaudible)hatuoni MP na ni watu.

Com. Lethome: Sasa unataka MP ambaye haonekani kwa constituency yake?

Okicha Duba: Tunataka anaye onekana.

Com. Lethome: Achukuliwe hatua gani yule ambaye aonekani?

Okicha Duba: Achukuliwe hatua ya kutolew na kuwekwe mwingine yule anaweza simamia hapo hapo

Com. Lethme: Haya endelea, endelea.

Okicha Duba: Ya pili, ya tano

Com. Lethome: Ngojeni tuendele, ngoja tuendele.

Okicha Duba: Kama ni mbaya sasa ya mwisho,

Com. Lethome: Unajua ina recordiwa hii sasa ukifanya kelele kidogo tu alafu tunaendelea isirecord kelele nyingi. Haya.

Okicha Duba: Ya mwisho, afadhali tuwe kitu kimoja, tusiwe na kabila kila mtu tushikane hiyo ndio amri tafadhali tuweke.

Com. Lethome: Kwa hivyo wewe hutaki mambo ya Borana province?

Okicha Duba: Aa hapa sisi tuko pamoja .

Com. Lethome: Haya sawa, asante. Peleka maoni yako huko asante sana Bwana Okicha. Haya Mohammed Abdi, Mohammed Abdi huyu ni kijana mdogo.

Mohammed Abdi: Kwa majina naitwa Mohammed Abdi Alake, hamjamboni nyote hapa?

Audience: Hatujambo.

Mohammed Abdi: Nawakilisha vijana. Katika division hii yetu ya Merti ile shida wako naye, napendekezo ambaye tungetaka tuwekewe katika Katiba mpya. The Constitution should provide us with a free copy of Constitutional document to every Kenyan for easy understanding. To enhance better comprehension it should be drafted in simple and clear expressions. The Constitution should cater for unemployment by rising of per capital income; the Government should entitle an individual virtually by being a citizen to the right of earning.

The new Constitution should entitle each and every one to equal free, affordable education up to O level system. The Constitution should ensure that the Higher Education Loans Board should extend their help also to self-sponsored students and offers the loans equally without biaseness. The Constitution should ensure the ideas of cost sharing by most public hospitals and clinics and income should be scrapped off. The terms of job, the terms of experience in most jobs requirements in our most public press and medias should require a consideration. We therefore require an establishment of such long period of experience in both public and private premises. The chances of Councillors should be based on academics matters and elected Councillor must own an O level certificate. The place of the district Commissioner in provincial administration should be a chance of an elected member by the people not a ial appointee.

The present system of education that is 8-4-4 should be eroded and the former that is 7-4-3 to be brought in files. Female genital mutilation idea of practice should be completely abolished and parties in breach should be accordingly handled. The distribution of National resource or cake should be fully exploited and as we have, benefit the particular community or society of the endowed region. The Constitution should provide total free movement in the country irrespective of tribal, religion or political stand. The Constitution should allow and recognize us on all aspects of development that is: social, political, and economical. The Constitution should entitle us to enjoy equally the efforts of our leaders.

The Constitution should provide different consideration in various job requirements. The cases of collective punishment should be abolished, incase someone violates the court he or she should be sort and dealt with accordingly. The issue of the essential document for instance identity cards, birth certificate and passport should be issued freely, equally and accesible through simple procedures. Passport particularly should be decentralized up to the district level, from the headquarter while birth certificate to be in provincial and common dispensary levels. Thank you.

Com. Lethome: Asante sana Mohammed. Tupate Dika Wario.

Dika Wario: Salaam Aleikum, mini kwa majina naitwa Dika Wario Mbuna, nafikiri Bwana Chairman hata ukisema sisi tunazungumza tu mambo ya ardhi hiyo ndio shida yetu kabisa, hapa ile kitu natukula moyo ni mambo ya usalama, mambo ya ardhi, pamoja na mambo ya ukosefu ya soko kwa mali yetu. Hiyo ndiyo tunaongea. Nafikiri hiyo ingine imebaki kuna watu wamepanga wameandika wataongea juu ya hiyo.

Com. Lethome: Sawa.

Dika Wario: Nikianzia, nafikiri hiyo vile wameongea hiyo ndio maoni yetu ama mapendekezo yetu. Sisi jamii ya Borana nafikiri tumeachwa nyuma kabisa kusema ukweli, hasa sisi ni watu wa mifugo, mifugo yetu tunaona iko dhuluma hatuna soko, hatuna dhamana, vile mnajua kila kitu iko na board yake, hatuna board. Sasa mapendekezo hapa ama maombi lazima tuwe na board, ya livestock na mali yetu iwe na soko mzuri. Katika Katiba mpya tuhusishwe sisi kama Wanakenya tuwe na kama Wakenya wengine kiKatiba. Kwa hivyo hiyo ndio maombi yangu. Hiyo ingine naunga mkono vile wale wa kwanza waliongea mambo ya Borana province sababu sisi tumemezwa na wale matajiri ambao wako na kahawa, wako na majani ya chai, wako na barabara ya lami sisi tumebaki watu wa nchi kavu tuwe na province moja kwa sababu shida yetu ni moja. Kwahivyo mimi mapendekezo yangu ni hayo tu asante sana.

Com. Lethome: Sasa hii Borana province itakuwa na uhusiano gani na ile Serikali ya katikati ile Serikali kubwa kutakuwa na uhusiano gani?

Dika Wario: Tuko na uhusiano kama sehemu ingine kama vile sasa tuko, tuko na uhusiano mzuri tu vile tuko hata sasa tutakuwa na uhusiano mzuri.

Com. Lethome: Okay. Na kwa mfano kama kuna mtu ambaye si Mborana lakini ako na mali na ako na ardhi pengine amenunua plot yake ama shamba yake katika hiyo province, ntu kama huyo atafanyiwa nini kwa sababu hivi sasa watu wanaogopa mambo ya ukabila wakizungumza habari ya majimbo.

Dika Wario: Hiyo sasa ataishi vile Katiba mpya itatengenezwa.

Com. Lethome: Wewe unataka iseme nini? Nataka maoni yako sasa hiyo Katiba mpya itatengemea maoni yako sasa.

Dika Wario: Sasa maoni yangu, aondoke aende province yake hii apigie Borana.

Com. Lethome: Maoni yake hayo asante. Sheikh Hokile, hebu tuendeleeni, tuendeleeni Sheikh Hokile ndio tulisema asubuhi

kila moja ako na uhuru ya kusema vile anataka.

Sheikh Hokile: Wasalam aleikum alaham dulilahi wa barakatu. Basi mini nawakilisha jamii ya Waislamu katika Mert division lakini kabla ya kupitia kitu ambaye inahusu hasa Waislamu kidogo kuna general inahusu mambo ya federal system ambaye maoni sisi kama Waislamu ambayo tuna wakilisha Islamic organization na Waislamu kwa jumla hii mambo ya federal system ambaye ni majimbo hiyo ndiyo ambaye pia ni maoni yetu kwani hiyo system tunaona ukosefu ya mambo ya security sana sana imeletwa kwasababu ya watu kutojali maslahi ya community ya hiyo area, kwasababu wale ambao, wale, wale provincial administration ama armed forces kama police ama yeyote iko katika sehemu yetu hii Kasasan, wengi ni watu ambao kutoka sehemu ingine.

Hawawezi kujali masilahi ya hawa watu wa hii area kwahivyo sisi tunaonelea kama pengine tutakuwa na ile majimbo tunataka vijana wetu ambayo watakuwa katika hiyo area ambayo wanaweza kumaliza hii mambo ya insecurity hii problem ya usalama. Na pia vile sasa Serikali imetuweka pamoja na Eastern province ambayo sehemu nyingi ambayo iko tajiri kama Meru, Embu ama Wakamba, tunaona sisi hatufanani na hao katika kila hali na zile life style mambo ya economic background. Hatuhusiani na hawa watu. Kama share yetu ya Serikali ikija wao wako wengi ukipea wao wana-dominate economy yote wao wanachukua hawajali sisi katika sehemu. Ndio kwasababu ya hiyo sisi tuna hiyo right tuwe na majimbo yetu kando ama tuwe na watu ambao atleast tunafanana kama Turkana ama Samburu ambao tunahusiana ili tuwe pamoja. Kwa maoni yangu pia watu ambao wako katikati yetu tunaishi pamoja kwa plot ama na nini hao wana haki kuketi na sisi tu hakuna problem.

Sisi hatutafukuza hawa ama nini kwasababu katika wakati sasa hata province zenyewe zimegawa kwa system ya community ya clan sort of kwasababu ukikuta Coast province, North Eastern province ni watu ambao wanaishi yaani zile life style zao wako pamoja na wanaishi na Serikali. Wanapata share yao kando na hiyo share wanapatia yaani hiyo community yao kwa hivyo na pia tunamaoni pia kuhusu sisi tunaona area yetu ya Isiolo district tumepata umaskini hali ya juu sana sana wakati ile, wakati ile baada ya independece kidogo tu tulikuwa na ile problem ambaye watu wote wanajua kama (inaudible)-----ambaye tumewekwa kama ng'ombe pamoja, ng'ombe zilichukuliwa zikamalizwa. Sisi tunaona hii new system ama new Constitution ya ile watu ambaye wamadhulumiwa lazima haki yao warejeshewe yaani waangaliwe hali yao kwasababu unakuta Government wametusahau hakuna njia, hakuna mali. Watu wakikula ile mali ambayo sisi tunayo hata ng'ombe, Serikali hawashughuliki nayo, haoni kama hiyo ni mali. Hii Serikali ni Serikali ya Agricultural Government hatujui, tunataka Serikali ya community yote kwasababu yaani katika hii community ya Kenya watu wote wana maoni yao kila moja wana life style yao lazima hii position yaani irespect hiyo haki. Kwa hivyo sasa mimi narudi kwa ile area ambaye inahusu Waislamu yaani haba. Inahusu Waislamu ambaye nimeandika kwa kidogo memo kidogo na ambaye nitasoma, nitasoma direct.

As a Constitution is for the people of a country, our new Constitution should consider seriously our religious faith customs cultures and values. The English common law or any alien culture shouldn't have preference over our religious and customary laws. It has to be understood that variety and differences are a common law of nature which functions through out all walks of

life no one has powers to change it. Our new Constitution should forward the principals of diversity, of equality, which gives people real freedom of change. The new Constitution should have provision for application of Islamic law for Muslims and any, any law applicable to Muslim must be in conformity with the teachings or dictation of Islam.

Citizenship; the new Constitution should guarantee all Kenyans easy access to passport, identity card, births certificate, job opportunity and any other benefit. Discrimination should not come in any form. Muslims converts who wish to change to Muslim names should not be subjected to untold discrimination. In terms of education, now in all our learning institutions Muslim people or students must be availed an opportunity to study IRE which should not be substituted with any other subject. The students should select uniforms of their choice that is: Hejab for Muslim girls and trousers for Muslim boys. On Fridays students should be released earlier to prepare for Friday prayers, the two Islamic Idd celebrations should be made a public holiday, no tuition or extra classes or extra any activities for Muslim students on week ends as they are supposed to attend madrasa or Islamic schools. During the holy month of Ramadhan, afternoon lessons should be abolished.

The Arabic studies from primary level should be introduced up to the university level. Civic education should be introduced in the schools curriculum this is the view of the Muslim community. So that that the community should learn their rights. Islamic religious education or subject should be taught by Muslim themselves not other person of different faiths. Affirmative action in Muslim schools to be introduced that is freedom of worship or freedom of religion. The new Constitution must accord Muslims a free hand to implement their religious obligations in Judiciary, economy and their way of life. The new Constitution should consider seriously our religious state, customs, values, and culture.

The Kadhis Court, the Kadhis Court structure to exist at par with other common law, types of courts thus the Kadhis Court be in the following level. The Kadhis Court first instance in every district two Kadhis High Court in every province. Three Kadhis Court of Appeal, the Kadhis Court will deal with all matters pertaining to Muslims including mosque or madarasa or organization conflicts. Issues of marriage or divorce certificate, an assistant Kadhi appointed by the chief Kadhi with consultation with the area Muslim community should be in place every division. Muslim interest free bank or monetary institutions this is another topic, Muslim interest free bank or monetary institution the new Constitution to allow Muslims to have interest free bank to conduct business in accordance with the Muslim law. The Muslim code of dress, Muslims have a cord of dress of which a new Constitution should recognize as part of worship for Muslims

Com. Lethome: That shows what you do is this, just highlight the main points because we are going to receive that memorandum we cant allow you to read the whole of it please.

Sheikh Hokile: I am finishing, accordingly Muslim women or girls should dress in hijab both in learning institutions and work places as for male students people pupils in our learning institution should put on trousers thank you very much. Salaam Aleikum.

Com. Lethome: Just a minute Sheikh kuna kuzungumzia habari ya freedom of worship katika Katiba na unajua hata ile Katiba tuko nayo hivi sasa imetoa uhuru wa kuabudu lakini mimi nikiamua sasa nitakuwa sasa nitakuwa nikiabudu shetani alafu ile tunasema devil worship sinitarudi kwenye Katiba niseme Katiba imenipatia freedom of worship and my worship is to the devil. Sijui ungependa kusema nini hapo kuhusu freedom of worship.

Sheikh Hakile: Freedom of worship kama Muslim community sisi tunahaki yetu ya kuabudu I mean kuwa na kupata ile freedom of worship na kama kuna watu ambaye wataleta kitu kama hiyo unasema devil worship kama kitu hiyo si kitu ambaye wanatumia ama wao wanapractise ina affect hata wao ama ina affect community ni kitu ambaye inakusudiwa lakini kama Christian community or Islamic organization I mean Islamic community ambaye dini ambayo imejulikana duniani.

Interjection. Com.Lethome: Kwa hivyo ungependa tudefine who is to be worshiped in this freedom of worship?

Sheikh Hakile: Yes who is to be worshipped?

Com. Lethome: Okay?

Sheikh Hakile: Yes

Com. Lethome: Who? In your opinion?

Sheikh Hakile: God.

Com. Lethome: Okay. Asante. Tunaendelea Hassan Wako, Hassan Wako.

Hassan Wako: Kwa jina mimi ni Hassan Wako, Bwana Commissioner nakushukuru mimi hapa kwa kufika hapa. Ningependa kuzungumza kidogo juu ya Constitution ya mbele, hii Constitution ya mbele ambayo sii yetu imeumiza Kenya hii.

Interjection. Com. Lethome: Karibia Hassan kidogo.

Hassan Wako: Kiwango inawezekana nafikiri tutaenda mbali na hiyo Constitution kwasababu hiyo ya mkoloni watu wa Kenya bado husika sasa tunataka ile yetu. Na sasa tukisema ile yetu tunataka ile yetu iwe namna gani alafu itusaidie tunataka iwe simple, tunataka iwe precise, tunataka free from complexity, tunataka iwe free from ambiguity, tunataka watu wote Wakenya wasomeshwe juu yake, tunataka watu wa Kenya wote waheshimu hiyo Katiba, tunataka watu wa Kenya wote waifuate hiyo Katiba tunataka hiyo Katiba iwe na self guard ndani yake, self guard ambayo hakuna jinsi itasumbuliwa kwani iwe kama ni

kuwa ammended, kuwe na referendum. kama ni kuweka mambo ingine iwe ni referendum, iwe ni Katiba yetu ya Kenya na hiyo ndiyo Katiba tutakayo sisi.

Je nini tutaandika katika hiyo Katiba? Tunataka Katiba hiyo mpya iwe na strong wording na iwe na strong wording on land sababu tatizo la nchi ya Kenya kwa jumla utasema utakuta ni ardhi ile tunapigana, ile tunakufa, ni juu ya ardhi. Kwa hivyo iwe na strong wording na area of representing juu ya ardhi. Property ni ingine siyo tu wording kuandika property lakini property iheshimiwe na iwe na haki kamili. Alafu maisha ya binadamu ambayo imepoteza dhamana lazima iwe na dhamana. Kitu ya nne ambaye tunataka kuona juu ya hapo ni rights haki, haki ya watu ya aina yote sasa mbele ya kuendelea na ingine nataka kusema yetu.

Mbele ya kwenda Kenya sisi tunataka nini? Sisi tunataka affirmative action. Katika affirmative action tunataka kusema ya kwamba sisi miaka hii thelathini ya uhuru Kenya ilipopata yetu ilipotea, mkoloni alitupa uhuru lakini Kenya iliondoa. Constitution iliharibu watu. Sisi nataka kupewa ile uhuru vile tulikuwa tukikaa. Uhuru wapi? Uhuru juu ya ardhi yetu, uhuru katika shamba yetu, uhuru katika mali yetu, uhuru katika masomo, masomo ambayo tutaweza kupata nayo kazi, hii masomo tumesoma ndani ya Kenya haijampa sisi kazi, hata kama nasoma sisi na watu wetu napata degree hata kama iko na degree ya p ili hakuna kitu tunapata. Inahusika hata mpaka Commission kwasababu hakuna mtu yetu ndani kwasababu ya ile ubaguzi na kukosa nitaendelea.

Tunataka Katiba ambaye itaandika reconstruction kama kitu kusha haribiwa if you have destroyed something lazima unareconstruct lazima unjenge upya, ile kitu wakoloni walijengea sisi hatuna sasa, maji kama iko, imepotea. Skuli kama iko imekuwa mbaya sana, hospitali kama iko haina dawa imekufa, so yote hata police station irudishwe ijengwe mpya, reconstruction ndani ya hiyo Constitution kama hatutaona hiyo maneno sisi hatuwezi tosheka.

Ile ingine tunataka restitution, restitution katika sheria ni kusema unarudisha mimi pahali nilikuwa, pahali nilikuwa ni tajiri katika East Africa mzima kuliko kila mtu ukiangalia katika kitabu na hiyo imepotezwa wakati uhuru ulifika ilirudisha mimi pale nikae vile nilikaa. Pia uandike rehabilitation sisi nataka rehabilitation hapana watoto hata sisi wote mmetuharibu, umetuharibu kwasababu ya kumpa sisi mahindi, kuharibu sisi kwasababu lazima tuishi na mahindi na sio kwa jasho letu sisi nataka rehabilitation. Tunataka pia restoration katika hiyo maneno na tunataka compensation word compensation must be there, na word marshall plan must be there marshall plan, tunataka marshall plan iweko ili watu waweze kuendelea na hiyo.

Interjection. Com. Lethome: Wee eleza zaidi marshall plan tafadhali.

Hassan Wako: Marshall plan plan ambayo itakuwa rasmi kwa sehemu hizi za northern Kenya, rasmi muweze kuweka amani yote, nguvu yote kila kitu ili maendeleo iwepo na ikae kama nchi ingine ya Kenya. (inaudible) alafu siyo hiyo pekee yake mimi naona ubaya yetu na tatizo yetu ilitokana na ile makosa ya kwanza tulifanya. Sisi tulisamehe Kenya, Kenya bado samehe sisi.

Kenya bado samehe sisi mpaka sasa kwa hivyo wanaendelea kunyanyasa sisi na kutupa taabu na kila kitu wanafanya mbaya kwetu kwahivyo tunahitaji reconciliation iandikwe huko kuna sehemu nataka reconciliation sehemu ambayo inataka Commission iwekwe kando iangalie juu ya usalama wetu na iangalie juu ya reconciliation ili tupatane rasmi mwaka wa seventy eight tulifikiria tumepatana lakini bado, bado samehewa sisi tulisamehe Kenya Serikali tulipigia kura tangu sixty three mpaka leo sisi bado badilisha kura yetu hata leo KANU inahesabu ni yake lakini sasa huyu mtu ambaye unahesabu ni wako na humsaidii kwa chochote namna gani.

Hata Moi alipo tuambia tuchunge nchi ya Kenya tulimuambia je, wachungaji wanakamuanga ng'ombe sasa sisi hii ng'ombe yetu ya Kenya tunapata nini ndani yake ili tuchunge? Kwahivyo lazima tupate kitu ya, kupata kitu ndani ya nchi ya Kenya kama sivyo haina maana. Haya sasa nyuma ya hiyo tukiendelea mbele nilifikiria juu ya hizi basic right iweko, hizi basic right iwe kamili halafu juu ya hiyo security, social right, political right, economical right, minority right, iweko, indigenous people rights iweko na haki ya hawa watu wasio jiweza wakina mama, vijana na watoto.

Juu ya minority right Commission wakati moja iliniuliza kama naweza kuja nayo saa hii nitapeana leo inasema declaration of the right of persons belonging to National ethnic, religious, linguistic, minorities UN declaration nitabeba kwa kikundi yako kwa sababu hii waliuliza safari ingine sasa mtaenda nayo, mtajua ni nini ninasema na sitaki kuingilia mtajua. Alafu nilisema haki ya indegenious people, juu ya indegenious people haki yake pia nimekuletea inasema nini haki ya watu ambao wako vile vile ukubwa ya hii maneno ni ya kwamba wanadhamini ardhi yao. Mchezo ya ardhi hii, itamaliza sisi, sisi hawezi wachana na ardhi yetu hata kipade kidogo kwahivyo hiyo pia nimekuletea nitawacha na wewe, sasa hiyo ni juu ya rights.

Sasa region, mimi nafikiria lazima kuwe na hiyo region wazee nasema, na pia jina isijalishe wewe bandika jina ile mnafikiria lakini ni region ambaye itakuwa na Marsabit, Isiolo, na Moyale. Kama jina yetu itakula ile jina ya Borana, itakula kitabu ya Kenya wachana naye hapana andika Borana, kama hapana kula uweke. Sasa ingine nataka stronger local Government Serikali ya ndani iwe. Sasa nakuja kwa maneno ya ardhi na boundary wazee walizungumza maneno muhimu ya boundary, boundary ilichezwa naye kila minister yule wa ardhi alikuja akajikatia kidogo ardhi ya wenyewe. Sisi tumepotesa ardhi yetu kutoka mahali wanaita huko Subuika kuja mpaka Isiolo town ilipotea. Imenyakuliwa sasa watu ingine wako ndani sisi tasamehe wacha kakaa hapo lakini wajiite Isiolo hata hawa. Hapana jiita nchi ya Meru.

Wengine wanaanza kunyakua pande hii nasema ni Wajir sisi najua pahali yetu ni (inaudible) hiyo ndiyo mpaka yetu kama wanakaa hapo wajiite watu wa Isiolo hapana nchi ya watu ingine. Na kuingineo hapa upande ya Garba Tula pia sehemu ingine ilipotea kwa hivyo boundary ya mkoloni iheshimiwe na iwe hiyo na iangaliwe kabisa kama ni kurudia kurudia rudisha.

Haya, tumetoka kwa boundary sasa naongea juu ya ardhi yenyewe isije tena kamwe iwe kitu ya biashara hii ndio imeharibu Kenya hii ndiyo tunamalisiana juu yake ardhi isiwe kitu ya biashara, ardhi isiwe kitu ya kuuzwa uzwa kila mahali ardhi iwe ardhi ya watu wa Kenya kukaa namna hiyo hapana kuuzauza kwahivyo hakuna kuuza ardhi hii title deed siyo ya kuuza vitu iwe ni ya

watu kuka nayo. Ardhi hasa ya watu hawa hakuna kuuzwa nataka hiyo Constitution nasema personal land no selling no value attached it is our land we want to remain with it we remain in it hiyo ndiyo. Sasa naendelea kwa hii maneno tunaita freedom of movement, freedom of movement ndio Constitution nasema hivo hata hii iseme lakini iwe na boundary hapana kumove na ng'ombe yako yote nalete hapa sisi hapana sikizana juu ya hiyo freedom of movement doesn't mean that it means I move anywhere in Kenya. I do not move all the Borana from here and take them to Sikutamama, we are only thirty thousand people so with that freedom if people move with all the animals here and this people will move here with all their people then we lose the true right that we have.

That small political right we have in peace we lose them, most of them we have Councillors we shall loss all of them we already have more than six in Isiolo town we don't have our Councillors they have been taken by other people. A move is on to take even this ones so minority will suffer at the hand of Government if there allow freedom together with movement of things and also buying property, buying property elsewhere no, rent them, live in them, do anything, do your business but don't buy. No ownwership of land in other peoples land you own in your land you have land live there iandikwe ndani ya hiyo Constitution hata iandikwe hapa.

Identity card, you get identity card in your district not in other districts. Kwenu kila mtu aende kwake apate card yake hapana kwa hapa kwasababu minority kama naandikisha watu thirty thousand tosha uhuru yetu napotea. Haya kura, hata kura kwenda kwako piga huko tu, pigia watu wako wawe wajumbe, chagua wako tu hapana chagulia sisi, sisi nataka mjumbe yetu wengine naingia hapa wengi nampa sisi ile mtu atamaliza sisi. Kila wakati imefanyika namna hivyo we want this man they want this other man now we loss our rights so you vote in your district don't vote in this district. For Kenya, I am saying.

Birth certificate you go back to your place of birth even if you are born in Isiolo it must be written born in Isiolo but originally from kisii. Born in Isiolo originally from Mandera this is to make Kenya for Kenyans not Kenya for other people. In Kenya here right now you go most a lot of people in Nairobi are not from Kenya and all the children are born here you loss employment opportunities for our people watu wanakuwa mara moja, walewalizaliwa wakati wa uhuru ni wazee waliingia kazi naingia kazi na jina yetu sisi nakosa kazi wao napata haki sasa maneno gani haya kila mahali namna hiyo sio sisi peke yetu hata kila mtu utakuta namna hiyo tu taabu watu ile nakuja napata, wanapata ile passport, wanapata kazi sisi hakuna kitu.

Com. Lethome: Mr Hassan sum up please

Hassan Wako: Mkubwa nina bakisha maneno chache ambayo ni ya muhimu mimi nafikiri basi mimi nasema sasa juu ya , asiwe above the law hiyo powers trim, punguza nakubaliana na wale walisema vice achaguliwe siyo na bunge na watu awe running mate kwa . Nina maneno juu ya MPs, wajumbe hakuna ndani ya mkono ya watu wa Kenya, sisi natupa kura hata sisi nasumbua lakini mwisho yao hiyo. Sisi hapana kosana natakiwa wabunge iko ndani ya wananchi kama nakosa iko njia mbaya awe arudi hapa if possible mara moja haraka hapana ongojea maika tano. Kusumbua watu miaka tano hakuna haki kitu hii ni

mambo kujaribu kama sisi nachagua mtu mbaya ye mamalisa sisi hapana wakilisha miaka tano miaka mbili ondoa kwetu.

Halafu Councillors pia hali iwe namna hiyo ile ya nomination, nitaenda kwa nomination, nomination hapana yakuweka watu ya KANU, watu ya NDP namna hiyo hapana nomination ni haki ya wale wasiyo na MP katika Kenya. Wako watu kama hawa tangu uhuru mpaka leo district hii bado pata nomination ile. Ile inaitwa nominated MP to this day, thirty years never hata mkono ya rais kusha kata kuandika jina yetu kwa nini rais naandika mkubwa ya civil service sisi hapana iko ndani rais naandikanga wakubwa ya board sisi hakuna ndani hata moja, rais naandika Commission na sisi hapana iko ndani sasa yeye hapana wacha hiyo hata harambee rais bado fika Isiolo district mpaka leo miaka thelathini sasa miaka thelathini Kenya nzima najengewa na harambee hata rais wetu bado fanyia sisi mambo faida gani hii? Sisi tuko na shida, hiyo shida yetu hiyo Constitution tutachagua mayors na Chairman wawe elected.

Sasa hii ingine Constitution hii iandikwe it guarantees equitable distribution of resources hata pesa kila district apate yake kamili kando hapana weka sisi. Tena hapa kuleta na kurudi naye hiyo ndiyo taabu yetu kubwa hiyo kitu pesa tunapewa inakuja hapa inachukua inaenda nayo sasa kama naenda nayo faida gani tena, kama DC kusha enda nayo kama PC kusha enda naye, kama head of department kusha enda na pesa yao that is our problem. Mwisho nikisema.

Intetjection. Com. Lethome: Can you, can you please elaborate hiyo kuenda nayo inakuwa vipi?

Hassan Wako: Yes kuenda naye, kuenda naye ni hii grabbing ya pesa ya Serikali ile kitu ya Serikali yote iko hata nyumba ya Serikali yote watu wamechukua hivo hivo ndio wanaenda naye hata wengine wanachukua, hata pesa yetu kama sisi nachanga harambee wengi kwisha enda naye. Wacha ya Serikali hata yetu mara kwa mara sisi sasa tumefika karibu na mwisho ile nitasema university (inaudible) Muslim issues hii hapa ndio iko shida (inaudible) kwa Waislamu kwanza imeanza kuwa taabu hata saa hii vile tulivyo we (inaudible) wanasema ni maendeleo wanakuja wanasema mimi tuko njaa lazima (inaudible) hiyo ni maneno mbovu mtu.....

Interjection. Com. Lethome: Wewe sasa fanya hivi mimi nataka tu pendekezo tafadhali don't mention other people yes.

Hassan Wako: Religious holiday, sisi nataka dini yote iwe na holiday yao, na iwe recognized by the Government. Freedom of worship sisi nasema iwe recognized ni kama iko. Sisi tunataka kuadhimu saa kumi na moja ya usiku watu nasema ninyi napiga kelele usiku kwa hivo hakuna ruhusa na mara mingi tunakataswa mimi kisha kuwa katika musikiti huko Nairobi karibu na administration police hakuna. Ninekuwa musikiti ingine huko hakuna nakataswa, nakataswa kwa nini na freedom of worship kama iko? Haya freedom of expression pia isiyoruhusu watu wengine kuto ingilia ndani ya misikiti na kanisa bila ruhusa bila kufuata njia kwa sababu mara mingi misikiti yetu (inaudible) kwa njia kama hiyo haya sasa hiyo iandike values ile ambayo tunahitaji ndani ya Constitution, justice, equality for all Kenyans, human development, unity welfare of disadvantaged group. Mwisho wakati nasema marshal plan nilikuwa nataka kuwaambia kwanza wakitupa pesa hizi natoka kwa wanyama wetu ile

wanyama ya msituni, all Game Reserve are in this arid land pesa hiyo thirty percent iende kwa hizi masoplan ile pesa ya soko mambo ya stima, stima yote ya Kenya inatokanga ndani ya mto yetu. Ningependa kushukuru Commissioner na, wananchi kwa kukuja kwa jumla, nafikiria tuko wengi sana. Niko na proposal kuhusu governance. Niko na maoni 13, sasa nitataja moja kwa moja. Ningependa kusoma kwa lugha ya kimombo sijui kama ninaweza pewa nafasi.

Com. Lethome: I think it is difficult to the people.

Hassan Wako: Kwasababu wengi hawaelewe hii lugha lakini bado nitasoma tu kwa Kizungu.

Com. Lethome: Wewe soma kwa Kizungu kwasababu it is meant for us not for them.

